



MSAADA KWA WATU WAZIMA

**SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI
KWA AJILI YA WAATHIRIKA WA
USAIFIRISHAJI WA BINADAMU**


Mwombe kijana asome Yohana 10:10: '....mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.'

Umewahi kuibiwa chochote kutoka nyumbani kwako au kwa mtu wako? Hilo lilikufanya ujisikie vipi? Je, kilichoibiwa ulikipata?

Vitu vingine vinavyoibiwa tunaweza kupata vingine vya mfano wake. Lakini vitu vingine tulivyo navyo ni vitu maalum kwasababu vitu hivyo ni sehemu yetu, vinatufanya tuwe tulivyo. Vinapoibiwa, inakuwa vigumu kuvipata vingine. Vitu hivi vinaweza kuwa ni vitu gani?

Njia moja ya kuelezea kikamilifu sisi ni nani ni kupitia kwa picha ya nyumba. Nyumba hujengwa ikiwa imeungana na ardhi. Huonyesha muungano wa kina kuhusu mahali petu. Kuta za nyumba zinaweza kujengwa kuzunguka nguzo nne. Hizi hufanya imara maisha yetu. Hali yetu njema ya kiafya, kiakili na kihisia, afya yetu njema ya kiroho na afya njema ya familia yetu na jamii yetu. Kama watu, muunganiko wetu husaidia kutoa umbo la sisi ni nani na hutufanya tudumu katika afya njema. Hutuwezesha tuishi maisha makamilifu.

NGUZO NNE ZA HAUORA YETU



(Umba upya picha hii, na hiyo picha iweke kwa jina la Sir Mason Durie, Te Whare Tapa Whā, 1984)

Biblia imejaa hadithi zinazolezea mwanga na giza lililomo katika dunia, matokeo ya mwanguko. Mwizi anayeelezwa katika Yohana 10:10 haji kutuibia vitu vyetu halisia tuvionavyo, bali huja kutuibia vile vilivyo vya thamani sana kwetu: maisha makamilifu aliyotaka Mungu tuwe nayo. Unafahamu mambo gani yanayotuwezesha kuishi maisha makamilifu? (Mifano mingine inaweza kuwa furaha, utu, heshima.)

Yesu ni habari njema kwetu, kwasababu pendo lake na sadaka yake humaanisha hata kama tumenyang'anywa yaliyo ya thamani, anaahidi atayarejesha. Yeye anaweza kutupa maisha makamilifu, hata kama tukjisikia tumeyapoteza.

(Soma mfano wa Kondoo Aliyepotea)

Utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu (UKUHB) ni tendo la kumnyang'anya mtu moja ya kitu chake cha thamani sana: uhuru wake. UKUHB huwadanganya watu na kuwalazimisha waingie katika kazi ambayo sio ya haki wala sio salama. Watu wengine huahidiwa maisha mazuri au kazi nzuri kumbe ni mtego nao huishia kufanya mambo mengine. Mtu anaweza kuwa mwathirika wa utumwa au usafirishaji haramu katika nchi hiyo hiyo anayoishi, au wakati mwininge, katika nchi nyingine.

Kuna mahali pengi watu wanaweza kuwa utumwani bila ya sisi kujuia. Mara nyingi huwa wanaogopa kumwambia yeoyote au huwa wameambiwa wasimwambie mtu yeoyote au wakimwambia mtu watafanyiwa jambo baya sana. Aina mbili za utumwa ni ule utumwa kwa ajili kazi na ule utumwa kwa ajili ya ngono. Hata hivyo, watu wanaweza vile vile wakasafirishwa na kuwekwa utumwani:

- Katika mashamba
- Katika meli za uvuvi
- Katika hoteli au katika nyumba za watu binafsi kama wafanyakazi
- Katika madanguro au katika utengenezaji wa picha za ngono
- Katika ndoa
- Katika viwanda
- Kama askari

Biblia inasema tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Mtu anapomuumiza mwengine, huwa anamuumiza Mungu. Watu wanao wasafirisha wengine au wanakuwa na watumwa huwa hawawatendei kwa heshima na utu ambaa Mungu alitupa sisi sote. UKUHB huondoa uhuru wa watu, furaha ya watu, nafasi za watu, tumaini la watu na vingi vingine. Haya humuumiza sana moyo wa Mungu. Mungu anatupenda sana ndiyo maana ameahidi kulturejeshea yote yaliyopotea. Lakini analolitaka Mungu zaidi ya yote ni kwamba mtu yeoyote asinyang'anywe maisha yake makamilifu. Mungu anatualika tushirikiane naye kuhakikisha watu wanayapata maisha aliywakusudia.



MSAADAA KWA WATU WAZIMA

SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI
KWA AJILI YA WAATHIRIKA WA
USAIFIRISHAJI WA BINADAMU

WAFUNDISHE VIJANA

Unaweza kufanya nini?

1. Zifahamu ishara

Jifunze ujue kutafuta ishara zipi zinazoweza kukuonyesha kwamba mtu hapa ananyonywa. Kuna mambo mengi ya kutizama, ikiwa ni pamoja na hali ya maisha ya watu, hali ya kazi na ukague kuona jinsi watu wazima wengine walioawazunguka wanavyowatendea. Jifunze namna ya kuwa salama kwenye mtandao. Wewe na wenzako mnawezaje kutanzana ili muwe salama?

2. Waambie wengine (tetea)

Ukishajua zile ishara, washirikishe wengine ili na wao wazijue pia. Hii husaidia kujenga jamii zilizo salama. Chunguza ujue kama mahali unapoishi kuna msaada kwa wanuszrika. Mahali pengine, ukimshuku mtu kuwa anaweza kuwa muathirika, unaweza kutoa taarifa.

Fanya kazi na kundi dogo katika jamii yako kuongeza ufahamu wa swala hili. Unaweza kufanya jambo fulani katika shule yenu, mahali pa kazi au kanisani.

3. Omba! Waombee viongozi wetu, ombea mashirika yanayowasaidia wanuszrika, waombee wanaoteseka. Omba watoto wote ambaa ni wa thamani wapate maisha makamilifu ya Mungu.

4. Uwe wewe! – Sote tumeumbwa tofauti na tunaweza kuleta jambo la kipekee ili kuleta tofauti. Vijana mara nyingi ndiyo wepesi kuleta mabadiliko. Hapa pana mifano kadhaa:

Rez Gardi: Rez alizaliwa katika kambi ya Umoja wa Mataifa ya wakimbizi. Alipokuwa mtoto familia yake ilikwenda New Zealand kama wakimbizi. Alisoma kwa bidii shulenii, ingawa wakati fulani alionewa. Alifiki kiwango cha kuwa mwana sheria na sasa huwatetea wakimbizi wengine wanaoweza kuwa hatarini.

Rosalie Fish: Rosalie alipokuwa shulenii huko Marekani, alikuwa mkimbaji mzuri sana. Alipofikia miaka 17, alishindana katika mashindano akiwa amevaa mkanda mwekundu usoni mwake wenye maandishi kuwakilisha na kueneza ufahamu juu ya wanawake asilia katika jamii yake na nchi yake ambaa wamepotea na waliouwawa. Alisema, 'Nikikimbia mbio kuhusu swala hili, watu watagundua swala hili.' Anaendelea kueneza ufahamu kila mara anapokimbia, na kueneza kwake ufahamu kumepata mwitikio wa kimataifa.

MASWALI YA MSHANGAO

Sijui nini ni cha kipekee kuhusu wewe?

Sijui nini kipo mbele zako sasa unachowenza kuvamia?

Sijui kama kuna jambo unamsikia Mungu akikwambia binafsi usaidie kukifanya?

SHUGHULI

Chora, tengeneza au zungumza juu ya nyumba. Fikiria nyumba hiyo ni wewe (au jamii yako).

Uliza:

- Nini huingia ndani ya nyumba kuipa nyumba uhai?
- Vitu gani vinaweza kuwa maalum kwako na mahali ulipo na nini unachothamini?
- Vitu gani maishani vinaweza kuitikisa nyumba? Au vinaweza kuifanya isiwe imara/isiwe na afya?
- Vitu gani vinaweza kusaidia kuilinda nyumba? Vinaweza kusaidia kuifanya iwe imara/ iwe yenye afya?

Imeandikwa na Captain Missy Ditchburn.